JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI KONDOA
JARIDA MAALUMU LA MWENGE WA UHURU 2024

30 Juni, 2024

# Mwenge wa Uhuru waridhishwa na miradi Halmashauri ya Mji Kondoa



Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Kondoa **Ndg. Said M. Majaliwa** akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa **Ndg. Shaaban Milao** mbele ya mkimbiza Mwenge kitaifa **Ndg. Godfrey E. Mnzava 1 Julai, 2024.**

## SERA YA UHARIRI

Madhumuni ya Jarida hili ni kuhabarisha na kuelimisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Mji Kondoa. Aidha Sera, Mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inafafanuliwa kupitia jarida hili. Isipokuwa pale inapokatazwa habari za Jarida la Halmashauri ya Mji Kondoa zinaweza kunukuliwa ili mradi Mhariri ajulishwe kwa maandishi.

**Bodi ya Uhariri**

Said Majaliwa

Hassan Mtamba

Sekela Mwasubila

Agnes Chekani

**Mawasiliano**

S.L.P 711 Kondoa

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255262360313

**Mitandao ya Kijamii**

www: kondoatc.go.tz

kondoatc

kondoatc

Barua Pepe
td@kondoatc.go.tz

# NENO KUTOKA KWA MKURUGENZI



Ndg. Said Mwemezi Majaliwa
Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Kondoa

Natoa shukrani za dhati kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutuma vijana mahiri na wazalendo kuweza kumuwakilisha kikamilifu kukimbiza Mwenge wa Uhuru nchi nzima na kuhakikisha wanafikisha ujumbe wa Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2024 kwa wananchi unaosema:- "**Tunza mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu**"

Pia natoa shukrani kwa viongozi wa Wilaya wakiongozwa na Jemedari Mahiri Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Fatma Almasi Nyangasa, Waheshimiwa Madiwani, Mbunge wa jimbo la Kondoa Mjini Mhe. Ally Makoa, Wakuu wa itifaki, Divisheni na watumishi wote kwa ujumla. Umuhimu wa kipekee kabisa kwa wananchi wa Halmashauri ya Kondoa Mji kwa ushirikiano mkubwa na mapokezi mazuri ya Mbio za Mwenge wa Uhuru 2024.

Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2024 umekimbizwa Km 132 katika tarafa mbili (2) yaani Kolo na Kondoa Mjini, ambapo umepitia Miradi **6** yenye thamani ya shilingi **1,555,182,064.00** miradi hiyo ni ya Sekta ya Afya shilingi **87,336,460** Maji shilingi **803,911,272.00** , Elimu Msingi shilingi **142,934,332.00**, Barabara shilingi **500,000,000** vijana shilingi **8,000,000** na mradi wa Msitu wa miyombo Hachwi shilingi **13,000,000.**

Katika fedha hizo Shilingi **bilioni 1.5** ni fedha kutoka Serikali Kuu, shilingi **milioni 9** ni fedha toka Halmashauri na shilingi **milioni 3** nguvu za wananchi.

Mwisho, niwashukuru sana wakimbiza Mwenge Kitaifa wakiongozwa na Ndugu **Gofrey E. Mnzava** na wakimbiza Mwenge kimkoa niseme maoni na ushauri wenu tumepokea na tunaenda kuufanyia kazi. Niwakaribishe tena katika Halmashauri ya Mji Kondoa.

# MAPOKEZI YA WAKIMBIZA MWENGE KITAIFA MAEGESHO YA MALORI BICHA



Ndg. Godfrey E. Mnzava
Kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa 2024



Ndg. Nussaibat H. Ahmed
Mkimbiza Mwenge Kitaifa 2024



Ndg. Maria F. Mapunda
Mkimbiza Mwenge Kitaifa 2024



Ndg. Makwaya J. Makwaya
Mkimbiza Mwenge Kitaifa 2024



Ndg. Ramadhani M. Khamis
Mkimbiza Mwenge Kitaifa 2024



Ndg. Claude A. Kilala
Mkimbiza Mwenge Kitaifa 2024

# MATUKIO KATIKA ENEO LA MAPOKEZI YA MWENGE STENDI YA MALORI BICHA



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Fatma A. Nyangasa (kulia) akikiri kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe. Janeth Mbene.



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Fatma A. Nyangasa (kushoto) akiwa na Katibu Tawala Ndg. Christina Kalekezi eneo la mapokezi Bicha



Mwenyekiti wa Halamshauri ya Mji Kondoa (wa kwanza kushoto) na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa wakiwa katika eneo la mapokezi Bicha.



Mbunge wa Kondoa Mjini Mhe. Juma Makoa (Kushoto) akiteta jambo na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kondoa Ndg. Hija Sulu wakati wa mapokezi ya Mwenge.



Viongozi mbalimbali waliojitokeza kwa ajili ya kuupokea Mwenge wa Uhuru katika eneo la maegesho ya Maroli Bicha



Mbunge wa viti Maalum Mkoa wa Dodoma Mhe. Mariam Ditopile akiwa katika eneo la maegesho Bicha kwaajili ya kuupokea Mwenge wa Uhuru .



Wananchi wa Halmashauri ya Mji Kondoa wali-ojitokeza kuulaki Mwenge wa Uhuru eneo la mapokezi Bicha



Sehemu ya watumishi wa Halmashauri ya Mji Kondoa waliojitokeza kuupokea Mwenge wa Uhuru eneo la maegesho Bicha.

# MATUKIO KATIKA ENEO LA MAPOKEZI BICHA MAEGESHO YA MAROLI



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Fatma Nyangasa akiongea eneo la mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Bicha kabla ya kuanza kuukimbiza Halmashauri ya Mji Kondoa



Diwani wa kata ya Serya Mhe. Kulwa Pazi akiwa ameushikilia Mwenge wa Uhuru ulipowasili eneo la maegesho ya malori Bicha



Diwani wa kata ya Kilimani Mhe. Issa Kambi akiwa ameushikilia Mwenge wa Uhuru ulipowasili eneo la maegesho ya malori Bicha



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kondoa Mhe. Mohamed Kiberenge akiwa ameushikilia Mwenge wa Uhuru ulipowasili eneo la maegesho ya malori Bicha



Diwani wa kata ya Kingale Mhe. Abushehe Mbuva wakati wa itifaki ya Mwenge sehemu ya mapokezi stendi ya malori Bicha



Diwani Viti Maalum Mhe. Besela Maunga wakati wa itifaki ya Mwenge sehemu ya mapokezi stendi ya malori Bicha



Meneja wa NMB Kondoa Ndg. Rasul Msangi wakati wa itifaki ya Mwenge sehemu ya mapokezi stendi ya malori Bicha



Mkimbiza Mwenge Kitaifa 2022 Ndg. Sahil Geraruma wakati wa itifaki ya Mwenge sehemu ya mapokezi stendi ya malori Bicha.

# MRADI WA KIKUNDI CHA VIJANA WAZALENDO




Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa Ndg. Godfrey Mnzava pamoja na viongozi wengine akiongea katika mradi wa vijana Wazalendo WISKWANTIS.



Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa Ndg. Godfrey Mnzava pamoja na viongozi wengine akikagua moja ya maduka ya mradi wa vijana Wazalendo WISKWANTIS



Mmoja wa vijana wa kikundi cha Wazalendo WISKWANTIS akikadidhi taarifa ya mradi kwa mkimbiza mwenge kitaifa Ndg. Godfery Mnzava

## MAELEZO YA MRADI

Kikundi cha Wazalendo kilianzishwa mwaka 2023 kikiwa na jumla ya wanachama watano (5) ambapo wanaume ni wanne (04) na mwanamke mmoja (01). Kikundi hiki kinapatikana katika Halmashauri ya Mji Kondoa, Kata ya Kilimani Mtaa wa Wiskwantis

Kikundi cha Wazalendo kilifanya usajili katika Halmashauri ya Mji Kondoa na kinatambulika kupitia namba ya usajili DOD/KON/VIJ/2023/0005 na kimefungua akaunti ya kikundi katika benki ya CRDB – Kondoa yenye namba 0133725065700 Shughuli kuu za mradi zikiwa ni biashara ya duka la rejareja na uuzaji wa nishati

Halmashauri imetoa mkopo wa Shilingi 8,000,000/= fedha zote zikiwa zimepatikana kupitia asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani ya Halmashauri kama mkopo

Kikundi hiki kimeshamaliza marejesho yote ya mkopo waliochukua ndani ya mwaka mmoja ambapo pia wameweza kuanzisha duka lingine kutokana na faida ya duka la kwanza na wamejiinua kiuchumi na kuhudumia familia zao.

# MRADI WA UJENZI WA ZAHANATI YA MTAA WA CHOKA



Mwenge ukiwasili katika mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Mtaa wa Choka.





Mganga Mkuu Dkt. Emiliana Donald akisoma taarifa ya mradi wa Zahanati ya Choka mbele ya Kiongozi wa mbio za Mwenge Ndg. Godfrey Mnzava kabla ya kuweka jiwe la Msingi .



Zahanati ya Mtaa wa Choka

## MAELEZO YA MRADI

Mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Mtaa wa Choka umetokana na Sera ya Wizara ya Afya ya kujenga Zahanati ya kutolea huduma za Afya katika kila Mtaa.Mradi huu umehusisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) huduma za mama na mtoto (RCH).

Mradi umelenga kusogeza huduma bora za Afya kwa wananchi wa Mtaa wa Choka ambao walikuwa wakitembea umbali wa km 6 kufuata huduma za matibabu na kupunguza vifo vya kinamama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka 05.

Mradi ulianza tarehe 30/03/2022 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 21/06/2024 kwa awamu ya kwanza. Ujenzi unatekelezwa kwa kuzingatia utaratibu wa Force Account ili kupunguza gharama, kuongeza ubora na ufanisi wa kazi.

Mradi umegharimu kiasi cha shilingi 87,336,460.00 fedha kutoka serikali kuu shilingi milioni 75, shilingi milioni 9.3 mapato ya ndani ya Halmashauri na shilingi milioni 3 nguvu za wananchi.

Kiongozi Mkimbiza Mwenge Ndg. Godfrey Mnzava aliagiza mradi huo kukamilika haraka ili uweze kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi wa Mtaa wa Choka na kuweka jiwe la msingi katika mradi huo.

# MRADI WA USAMBAZAJI MAJI MTAA WA HACHWI



Jiwe la msingi mradi wa maji Hachwi lililowekwa na Kiongozi wa mbio za Mwenge Ndg. Godfrey Mnzava



Mwenge wa Uhuru ukiwa katika mradi wa usambazaji maji Hachwi





## MAELEZO YA MRADI

Mradi wa usambazaji maji Mtaa wa Hachwi umehusisha ujenzi wa Tanki moja la kuhifadhi Maji lenye ujazo wa mita za ujazo 100, ujenzi wa nyumba ya pampu moja na ufungaji wa pampu inayotumia nishati ya jua, ujenzi wa vituo vya kuchotea maji kumi (10), utandazaji wa mabomba ya maji kwa umbali wa Mita 15,069, ujenzi wa vituo viwili vya kunyweshea mifugo na ujenzi wa Chombo cha watumia maji ngazi ya jamii (CBWSO).

Mradi umelenga kutoa huduma ya Majisafi na Salama kwa wakazi wapatao 2,470 wa Mtaa wa Hachwi na viunga vyake.

Mradi wa Maji Hachwi ulianza kutekelezwa 22.01.2022 na unatarajia kukamilika 24.07.2024. Mradi huu umetekelezwa na Mkandarasi SAJO CIVIL ENGINEERING AND BUILDING CONST COMP.

Mradi utagharimu kiasi cha Shilingi 803,911,272.00 fedha kutoka Serikali Kuu ambapo hadi sasa umetumia shilingi 349,021,500 na upo asilimia 90 ya utekelezaji.

Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru Ndg. Godfrey Mnzava amewahakikishia wananchi wa Hachwi kuwa mradi huo utakamilika kwa kuwa fedha zipo na utatoa huduma kama ilivyopangwa na kwa wakati.

# MRADI WA UJENZI BWENI SHULE YA MSINGI IBONI



Kiongozi wa mbio za Mwenge Ndg. Godfrey Mnzava akiongea kwenye mradi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum IS/M



Jiwe la uzinduzi



Wanafunzi wakisoma shairi



Wanafunzi wakionyesha jumbe mbalimbali za Mwenge

## MAELEZO YA MRADI

Mradi umelenga kuibua wanafunzi wenye mahitaji maalum waliokuwa wanafungiwa ndani pasipo kupewa nafasi ya kupata elimu kama wanafunzi wengine..

Mradi ulianza tarehe 25/09/2024 na umekamilika tarehe 23/06/2024. Ujenzi umetekelezwa kwa kuzingatia utaratibu wa Force Account ili kupunguza gharama, kuongeza ubora na ufanisi wa kazi na kuihusisha jamii katika utekelezaji wa mradi.

Mradi umegharimu kiasi cha Shilingi 142,934,332.00 ikiwa ni fedha kutoka kwa wahisani Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Kukamilika kwa Mradi kutaleta maendeleo ya kijamii, kisaikolojia na kielimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na kuwapatia fursa ya kujifunza na kuimarisha stadi za kujitegemea.

Aidha kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa aliwapongeza wanafunzi hao kwa umahiri wao waliouonyesha ikiwemo kuimba wimbo wa taifa kwa alama na kuwahakikishia kuwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan yupo pamoja nao na ndio maana anatoa fedha za kuboresha mazingira yao ya kujifunzia.

# MRADI WA UJENZI WA BARABARA YA GUBALI-BOLISA-IBONI



Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru akiangalia jiwe la msingi baada ya kuliweka. Katika mradi wa barara ya Gubai-Bolisa-Iboni



Ukaguzi wa daraja ikiwa ni sehemu ya mradi wa barabara



Mkuu wa Wilaya Mhe. Fatma Nyangasa akiongea kwenye mradi



Daraja lililowekewa jiwe la Msingi ikiwa ni sehemu ya barabara

## MAELEZO YA MRADI

Mradi umelenga kurahisisha huduma za usafirishaji pamoja na kuzifikia huduma za kijamii ambapo awali kulikuwa na changamoto kubwa ya kutopitika hasa msimu wa mvua.

Mradi ulianza tarehe 05/09/2023 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 04/03/2024 kutokana na mvua mkandarasi aliongezewa siku 150 hivyo unatarajia kukamilika tarehe 02/08/2024 na unatekelezwa na mkandarasi M/S MIA BROTHERS TANZANIA LTD.

Gharama za mradi huu ni shilingi 547,153,890 ambapo gharama ya mkataba ulioingiwa na mkandarasi kwa ajili ya mradi huu ilikuwa ni shilingi 547,153,890 ambapo hadi sasa jumla ya shilingi 368,548,480 zimekwishalipwa.

Kukamilika kwa Mradi kutafungua fursa zakiuchumi na kijamii kwa wananchi wa kata za Kondoa Mjini, Chemchem na Bolisa ambapo wataweza kusafirisha mazao yao hadi kufika kwenye masoko kirahisi.

Kiongozi wa mbio za Mwenge Ndg. Godfrey Mnzava ameweka jiwe la msingi katika mradi huo na kuagiza kukamilika kwa wakati kwa kuwa mvua zimeisha kwasasa.

# MRADI WA UTUNAJI WA MSITU WA ASILI WA MIOMBO HACHWI



Msitu wa asili wa miombo uliopo katika Mtaa wa Hachwi



Ukaguzi wa msitu na KUU ya Mkoa



Katibu Tawala Ndg. Christina Kalekezi akiongea na mmiliki wa msitu



Mkurugenzi Ndg. Said Majaliwa alipomtembelea mmiliki

## MAELEZO YA MRADI

Mradi umelenga kutunza mazingira ili kupata mvua za kutosha zitakazowezesha kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupelekea mazao yanayolimwa pembezoni mwa msitui kustawi vizuri ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya utunzaji mazingira kwa jamii kwa vitendo.

Mradi wa kutunza eneo la msitu wa asili ulianza mwaka 2012 kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Kondoa kupitia mtaalamau wa misitu wa Halmashauri kupitia ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kondoa pamoja na Serikali ya Mtaa wa Hachwi mmiliki aliweza kuunganishwa na Shirika binafsi la Lead Foundation kupitia mpango wa KISIKI HAI na na mafunzo zaidi ya utunzaji mazingira.

Gharama za mradi huu ni shilingi 13,000,000 ikiwa shilingi 4,000,000 ni thamani ya ardhi na shilingi 9,000,000 ni gharama za uendeshaji ikiwemo nguvu kazi ya kutengeneza miundombinu iliyopo kwenye msitu.

Kiongozi wa mbio za Mwenge Ndg. Godfrey Mnzava alitembelea msitu huo na kuwapongeza kwa utunzaji wake na kuwataka kuendelea kuutunza ili ulete manufaa katika jamii nzima.

# UPANDAJI MITI KATIKA MIRADI




Mkimbiza Mwenge kitaifa Ndg. Godfrey Mnzava akipanda mti kwenye mradi wa maji Hachwi



Mkuu wa Wilaya akipanda mti na mkimbiza Mwenge kitaifa




Mkurugenzi  akipanda mti na mkimbiza Mwenge kitaifa



Katibu Tawala akipanda mti na mkimbiza Mwenge kitaifa

## MITI 177 YAPANDWA SIKU YA MWENGE

Jumla ya miti 177 imepandwa na viongozi wa Mwenge na wilaya wakati wa mbio za Mwenge Halmashauri ya Mji katika maeneo ya miradi iliyopitiwa na mwenge wa Uhuru.

Upandaji wa miti umefanyika ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa agizo la Makamu wa Rais Mhe. Isidory Mpango la upandaji wa miti milioni 1.5 kila halmashauri na utekelezaji wa kauli mbiu ya Mwenge wa Uhuru ambayo imebeba ujumbe wa utunzaji wa mazingira na uchaguzi wa serikali za mitaa.

Miti hiyo imepandwa katika mradi wa maji Hachwi, eneo la ujumbe wa Mwenge Tura Sekondari na mradi wa bweni katika Shule ya Msingi Iboni.



Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Kondoa Mhe. Hija Sulu akipanda mti na mkimbiza Mwenge kitaifa.

# MATUKIO KATIKA ENEO LA MKESHA KATIKA VIWANJA VYA SABASABA




Mkimbiza Mwenge kitaifa Ndg. Godfrey Mnzava akiongea na wahudhuriaji wa kongamani la vijana katika uwanja wa Sabasaba.



Mkimbiza Mwenge kitaifa Ndg. Godfreya Mnzava akiongea na mratibu wa UKIMWI Hospitali ya Mji Kondoa katika uwanja wa Sabasaba




Mkimbiza Mwenge kitaifa Ndg. Godfreya Mnzava akiongea na mratibu wa huduma ya mama na mtoto katika Hospitali ya Mji Kondoa katika uwanja wa Sabsabasaba



Mkimbiza Mwenge kitaifa Ndg. Godfreya Mnzava akiongea na mratibu wa Malaria katika Hospitali ya Mji Kondoa katika uwanja wa Sabasaba



Mkimbiza Mwenge kitaifa Ndg. Godfreya Mnzava akiongea askari wa michoro ya mapangoni katika uwanja wa Sabasaba



Mkimbiza Mwenge kitaifa Ndg. Godfreya Mnzava akiwa meza kuu na viongozi wengine katika uwanja wa Sabasaba



Baadhi ya wanafunzi wa haraiki wakiwa katika uwanja wa Sabasaba kwa ajili ya kutoa ujumbe wa mwenge 2024.



Mkimbiza Mwenge kitaifa Ndg. Maria Mapunda akitoa ujumbe wa Mwenge katika uwanja wa mkesha viwanja vya Sabasaba.